

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

06

URAI A NA MAADILI

Muda: Saa 1:30

Jumatano , 21 Novemba 2018.

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu A na B zenyе jumla ya maswali **sita (6)**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Sehemu A ina alama **ishirini na sita (26)** na sehemu B ina alama **ishirini na nne (24)**

SEHEMU A (Alama 26)

1. Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku.
 - (i) Ipi kati ya tabia zifuatazo inaleta uharibifu wa mazingira?
A. Matumizi ya mbolea ya samadi C. kukata miti oyoo
B. Kumwagilia bustani maji D. Kufyeka nyasi []
 - (ii) Ni faida gani inatokana na matumizi ya chandarua wakati wa kulala?
A. Kuzuia ugonjwa wa kifua kikuu
B. Kuzuia ugonjwa wa malaria
C. Kuzuia ugonjwa wa kipindupindu
D. Kuzuia baridi wakati wa usiku []
 - (iii) Kitendo cha baadhi ya watoto kuzurura mitaani ni kiashiria cha
A. tabia ya unafiki c) tabia ya tamaa
B. tabia ya majungu d) tabia hatarishi []
 - (iv) Ni kwa nini watoto wanashauriwa kukataa kupokea fedha au zawadi kutoka kwa watu wasiowajua?
A. Kuzuia utajiri c) Kuepuka vishawishi
B. Kuzuia uzururaji d) Kuepuka uvivu. []
2. Jibu kipengele (i) - (iv) kwa kuoanisha majukumu yaliyoainishwa katika **Fungu A** na vyeo vya wahusika wa majukumu hayo katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

Fungu A	Herufi	Fungu B
(i) Husimamia mahudhurio na taaluma darasani pamoja na nidhamu.	[]	A. Kamati ya shule B. Mwalimu wa darasa
(ii) Hupanga na kusimamia mipango yote ya maendeleo katika shule.	[]	C. Mwalimu wa taaluma D. Mwalimu mkuu
(iii) Husimamia mahudhurio ya wanafunzi shulenii na kuhakikisha kuwa wamevaa sare za shule.	[]	E. Mwalimu wa nidhamu F. Kiranja mkuu
(iv) Husimamia shughuli zote za uendeshaji wa shule za kila siku.	[]	

3. Chagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.
- i) Kitendo cha kumwambia mtu alichokifanya sio sahihi ni _____ (kumuadhibu, kumkosoa, kudanganya)
 - ii) Kufanya kazi kwa pamoja inamaanisha _____ (kushirikiana, kubaguana, kuchukiana)
 - iii) Kufanya mambo mazuri uliyojipangia ni _____ (ubinafsi, nidhamu binafsi, woga)
 - iv) Nini hutumika kudhibiti tabia za wanafunzi shulenii? (nembo ya shule, mipaka ya shule, sheria za shule)

SEHEMU B (Alama 24)

4. Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuonesha matendo yanayoonesha **haki** au **wajibu** kwa kuweka alama ya (✓) kwenye sehemu inayohusika. Namba (i) imetolewa **kama mfano**.

Matendo	Haki	Wajibu
(i) Kulindwa	✓	
(ii) Kucheza michezo mbalimbali		
(iii) Kuwasaidia wakubwa na wadogo zako.		
(iv) Kupendwa na kupewa mahitaji ya msingi.		
(v) Kufanya kazi za shule.		

Swali la 5:

Chunguza picha na kisha jibu maswali yanayofuata.



Maswali:

- (i) Watu wanaoonekana katika picha wanafanya tendo gani?
- (ii) Ni kifaa gani cha muziki kinachoonekana kwenye picha?
- (iii) Kitendo cha Wazungu kushirikiana na
Waafrika kama inavyoonekana katika picha
kinaonyesha nini?
- (iv) Nini umuhimu wa kujifunza kitendo kinachoonekana
kwenye picha?

Swali la 6:

Soma kwa makini kifungu cha habari kisha jibu maswali yatakayofuata.

Amina ni mwanafunzi wa Darasa la Nne katika shule ya msingi

Kibo. Amina anaishi na shangazi yake ambaye ni tajiri sana.

*Siku zote Amina huenda shulenii bila kula chochote asubuhi wala
kupewa kitu cha kula wakati wa mapumziko kwa sababu ya
uchoyo wa shangazi yake. Siku moja rafiki yake aitwaye Joani
alimshawishi ili amwibie fedha shangazi yake. Amina alikataa na
kumwambia rafiki yake kuwa kuiba sio njia ya kutatua matatizo
yake. Amina aliendelea kusema, "Naamini iko siku moja
nitafanikiwa kwa kufanya bidii katika masomo yangu na shughuli
nyingine, halafu nitajitegemea na kuwasaidia wengine".*

Maswali:

- (i) Shangazi yake Amina ana tabia gani?
- (ii) Kwa nini Joani hakuwa rafiki mzuri?
- (iii) Nani alikuwa na mtazamo chanya kati ya Amina na Joani?
- (iv) Nani mwenye tabia inayofaa kuigwa kati ya shangazi,
Amina na Joani? Toa sababu moja.